**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 11 Agosti 2007.**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Mohamed S. Mwenguo
Mussa Omari
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Rashidi Saidi Karanji
Shabani Ramadhani
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

**Wageni**
Severin C Mhina – Executive Secretary, HUWATA
Luka E Makona – Chairman, HUWATA
Engelbert Nyoni – ITDP Tanzania

**Ushirika na HUWATA**
Wageni wawili toka HUWATA – chama cha Huduma ya wasafiri Tanzania. Waliitambulisha HUWATA. Ni shirika lisilo la kiserikali, lilianzishwa mwaka 1975 na dhumuni la kuelezea mambo ya usalama kwa wasafiri, (wakiwemo waenda kwa mguu, wapanda baiskeli, barabara au treni). Wanaeleza mambo ya usalama kutoka ajali na uhalifu. Wanashirikiana na serikali ikiwemo TANROADS. Walielezea idadi ya miradi ya usalama wanayoifanya wakati huu. Wana wafanyakazi 16 Dar es Salaam na wengine ofisi za mkoa. Mmoja wa wafanyakazi, Sebastian kolele, ana uzoefu na upanda Baiskeli. HUWATA ilitoa wazo la kunzisha leseni kwa mradi na mashirika ikiwemo SUMATRA.

Elaine na wanachama wengine walielezea UWABA na kazi zake. HUWATA na UWABA waliafiki vizuri kushiriki ana na kufanya kazi pamoja.

Elaine alifanya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi wa usalama barabarani kutoka wamba Memorial fund. Mwisho wa kukusanya pendekezo ni tarehe 31 Agusti 2007 iliamuliwa kwamba tungependaa mradi ukiwa na vipengele vitatu.

- Kufundisha wapanda baiskeli kwa ujumla wakiwa wanachama wa UWABA kuhusu upandaji baiskeli salama.
- Kufundisha wanafunzi wa sekondari kuhusu usalama na upandaji baiskeli.
- Kuhimiza waalimu wanaofundisha udereva kuwafundisha wanafunzi wao kuhusu haki za wapanda baiskeli.

Fedha hizo zitatumika kuwalipa watakaofundisha ili waandae vifaa vya kufundishia, majarida, kukodisha, kumbi na kulipa washiriki na kuwapa viburudisho wakati wote wa mafunzo.

Ilikubalika kwamba Elaine atakutana na Severin na Luka siku ya jumatatu mchana kuandaa pendekezo ili wajumbe walipitie kwenye mkutano wa jumamosi

**Msafara wa Baiskeli.**
Bwana Nyoni wa ITDP alihudhuria mkutano wetu ili kutuarifu kuhusu ITDP kuunga mkono msafara wa mwaka wa Baiskeli. Elaine aliuliza ufafanuzi zaidi kuhusu wajibu na uhusiano wa ITDP na AALOCOM. Bwana Nyoni alisema yeye ni mwajiri wa ITDP Tanzania. ITDP inashirikiana na AALOCOM na wanafanya kazi ofisi moja. Bwana mlamba ni katibu mtendaji wa AALOCOM na prosper alikuwa mwajiriwa wa AALOCOM ila kwa sasa amesafiri kimasomo. Mradi wa Baiskeli Califonia ni mradi wa ITDP.

Bwana Nyoni alisema kwamba kira sasa ITDP ina matatizo ya kifedha hivyo haitaweza kusaidia msafara mwaka huu. Uamuzi huo ulitolewa na mkurugenzi wa fedha wa ITDP New York.

Elaine na wajumbe wengine walisikitika. Tulikutana na Bradley na ITDP Africa kusini ambaye alitupa moyo kuanzisha msafara wa Baiskeli na kutuhakikishia kuwa ITDP ingekutusaidia kama mwaka jana. Tulipeleka pendekezo la mradi mwezi April na hatukupata jibu rasmi kutoka ITDP kuhusu bajeti ambayo tungetegemea, kwa kufuatilia tuliambiwa kwa ujumbe mfupi kuwa ITDP ingetusaidia. Bwana Nyoni hakuhudhuria vikao vya UWABA wala vya msafara wa baiskeli ingawa alikaribishwa, amefika leo ingawa pia amechelewa saa nzima. (Bwana Nyoni alisema alitingwa na mradi wa Baiskeli Calfronia) hakuna aliyekuwa akijibu barua pepe zetu, Bwana nyoni au Bradley jambo hili lilionekana ni ukosefu wa nidhamu kikazi na ITDP kukosa heshima kwa UWABA. Wajumbe wa UWABA walisikitishwa na kuiweka ITDP miongoni vielelezo. Vibaya kwa UWABA. Juma na bwana Mwenguo walielezea kusikitishwa kwao kuhusu jambo hili.

UWABA ilisema kwamba tayari imewasiliana na kampuni kadhaa na mashirika zikiwemo ya kutengeneza Guta, Mohammed Enterprises, Knight Support, Zantel, Ubalozi wa Uholanzi, Bakhresa na Celtel kuomba ufadhili, na wamehakikishiwa kupata Guta kama zawadi ya bahati nasibu ya msafara, ila hakuna msaada kifedha tumewasiliana pia na mbunge Azam Zungu ili awe mgeni rasmi. Bila ufadhili wa ITDP inakuwa vigumu kupata msaada pengine kwani wengine hawana uhakika ikiwa tukio litafanyika.

Bwana Nyoni aliulizwa ukubwa wa ITDP na akasema ina wafanyakazi 20 katika Afrika na Asia pamoja na Marekani. Elaine alisema kwamba kiasi cha fedha walichosema ni kiwango kidogo ambacho pengine watatumia kwa ndege – mikutano n.k. wanachama wa UWABA walisema ikiwa ITDP itachangia Tsh 300,000 na baiskeli mbili zitasaidia kuendelea ma mpango wetu.

Baada ya bwana nyoni kuondoka ilijadiliwa ikiwa tuendelee na mipango yetu ya msafara wa baiskeli au la. Ilikubalika kuwa tuendelee kutafuta ufadhili. Tukifanikiwa basi tutaendelea na mpango wetu. Ikiwa tutashindwa basi tutafanya msafara kwa wanachama wa UWABA pekee bila ukumbi au matangazo n.k.

Elaine alisema atajaribu kuwasiliana na Knight Support ila meneja alikuwa kwenye kikao. Atafuatilia tena wiki hii. Juma alitukumbusha kuwa tunatakiwa kukutana na mbunge Azan Zungu kati ya tarehe 18 na 20 mwezi huu atakaporudi kutoka bungeni, Dodoma

**Mchango wa IBike**

Juma aliarifu kuwa yassin wa IBike ameweka benki Tsh 400,000 (Akaunti ya UWABA) na ameangalia salio na kukuta imeingia wanachama walifurahi kwani hii itasaidia kuendelea na ununuzi wa samani za ofisi na Guta ili kuzalisha.

**Ofisi**

Tangu wiki iliyopita, Ally Saidi Mohamadi na Rahma Ali walinunua rangi kwa Tsh 10,000 na kupaka ofisi, ambapo sasa inaonekana nzuri.

Ally said Mohamed amekadiria gharama za kutengeneza rafu ya magazeti na mbao mbili za matangazo. Mbao za matangazo zinaweza kutengenezwa kwa chipboard, gharama za vifaa ni Tsh 30,000 na Tsh 38,000 kwa rafu za magazeti (kila moja futi 6 kwa 4). Ilikubalika kuwa juma na Elaine watatoa Tsh 60,000 kutoka benki siku ya jumatatu na Tsh 11,000 zilizotolewa mchango wiki iliyopita na kumkabidhi Ally Saidi Mohammed kununua vifaa ambaye alisema atatumia muda wake kufanya kazi bure.

Bwana mwenguo alisema itakuwa vizuri kuwalika viongozi wengine wa serikali za mitaa kwenye ufunguzi wa ofisi punde itakapokamilika. Alisema balozi wa nyumba kumi atatusaidia kushirikana na viongozi wengine eneo hilo.

Ilikubalika kununua guta wiki hii. Elaine na Juma watatoa fedha benki tsh 280,000. tulimpigia simu Mhe. Ngaja kumfahamisha kuwa jumanne saa 4 asubuhi tutafika keko kununua guta. Ilikubalika kuwa Juma na Jumanne watakutana nae na kununua guta.

Ilikubalika pia kuwa Jumanne atafute dereva wa guta aliyemwaminifu ili alete mapato ya guta kila siku.

**Sanduku la barua**

Juma alifuatilia maelezo zaidi kuhusu kufungua sanduku la barua katika posta ya magomeni wiki hii. Kufungua sanduku kwa shirika ni Tsh 37,000 kwa mara ya kwanza na Tsh 30,000 kwa miaka itakayofuata. Picha mbili kwa kila wajumbe wawili na hakuna nyaraka nyingine zinazohitajika

Mkutano ulijadiki ikiwa tufungue sanduku au la kutokana na gharama kubwa wajumbe baadhi walisema tutumie sanduku binafsi la Elaine au Meja lakini wajumbe wengi walisema ni bora kuwa na sanduku la UWABA. Bwana mwenguo alichangia Tsh 2,000 kama gharama za ufunguzi wa sanduku la barua. Ilikubalika kutoa fedha benki Tsh 35,000 ili Juma aende posta kufungua sanduku la barua.

Hii inakamilisha jumla ya fedha zilizotolewa benki kuwa 375,000.

**Mpango wa Usafirishaji Dar es Salaam.**
Filbert aliarifu kuwa alikwenda chuo cha usafirishaji dar es Salaam na kukutana na bwana wemba ambaye anahusika na mpango madhubuti wa usafirishaji na mkuu wa kitengo cha usalama barabarani. Alisema kwamba baiskeli, Guta na pikipiki hazikuwa zimehesabiwa kwenye zoezi uchunguzi wa barabara (Jambo hili Elaine aliambiwa na kiongozi wa uchunguzi wakati zoezi hilo lilipokuwa linafanywa) na alitupa karatasi magari mbalimbali yaliyojumuishwa ambapo aina yoyote ya baiskeli haikuhusishwa. Alisema baiskeli zitongezwa baadae. Iliamuliwa kwamba UWABA itaomba mkutano nae ili kujadili jambo hili na jinsi tutakavyoshiriki kwenye kitengo hiki au yeye ahudhurie mkutano wa UWABA.

**Barabara zilizo kwenye mpango wa ujenzi**
Elaine alifanikiwa kumpata bwana Nitti wa TANROADS makao makuu aliyesema angekuja kukutana nae saa 4 asubuhi siku ya jumatatu. Alisema kuwa ni bora kuwa na mkutano wa utangulizi badala ya kutoa mada kwa powerpoint jumatatu, ila tungejadili kufanya hivi wakati mwingine, Elaine , Juma , Paulo, Shukuru (aliyetuma ujumbe mfupi) na Sosthenes walikubali kwenda kwenye mkutano.